# LEARNING BY EAR

## ”WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA DHIDI YA MALARIA”

**KIPINDI CHA NNE: ” ISHARA ZINAPODUMU..... ”**

**SCRIPT: CHRISPIN MWAKIDEU**

**EDITOR: ANDREA SCHMIDT**

**ASSISTANT EDITOR: KATRIN OGUNSADE**

**HEATH EXPERT: DR. HEIDRUN HÜBNER**

**List of characters for episode 4:**

- MASIKA (40)
- BETTINA (34)
- KAREMBO (14)
- DAVID (14)
- MAMA DAVID (43)
- ZAWADI (INFANT, no actor)
- H/TEACHER (34) (female)
- KAREMBOS CLASS (14+)

**INTRO/NARRATOR (same voice)**

Hujambo kwa mara nyingine msikilizaji na karibu tena katika makala yetu ya Noa Bongo Jenga Maisha yakp katika mchezo wa kuigiza WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA-Ikiwa ni VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA MALARIA. Katika kipindi kilichopita Karembo alipata homa kali na alipomwambia mamake Betina akatafuta ushauri kwa sahiba wake mamake david ambaye hatambui matumizi ya dawa za kisasa. Wakati huohuo Masika, babake Karembo aliinyakuwa neti iliyotibiwa kwa dawa ya kuua wadudu hasa mbu na kuenda nayo kuvulia samaki na kurudi nyumbani na shehena ya samaki lakini aliwaacha Karembo na Zawadi wakavamiwa na mbu hatari wanaoambukiza malaria walioenea katika eneo hilo wanaloishi. Je, anapomeza tembe aina ya klorokwini na kujifunika ndani ya blanketi Karembo ataweza kupata nafuu kutokana na Malaria ? Tega sikio katika kipindi cha leo kwenye kisa kwa jina **” IWAPO ISHARA ZITAZIDI”**

**MUSIC INTERLUDE**

**<u>SCENE ONE: LAKESIDE, MASIKA FISHING.</u>**

**A-SFX: FEET MOVING IN WATER**

1. **MASIKA:** **(PULLING NET)**
Shabash! Hii neti ina miujiza.. utadhani ni smaku… sijawahi kunasa samaki wengi kiasi hiki Lakini mbona vidogo hivi?aah Samaki ni samaki! Wadogo au wakubwa! ,wa manjano au samawati… bora ni samaki! Sasa nawania soko kuwauza… alafu nirudi nyumbani kuwaaangalia wanangu nijue wanaendeleaje…

2. **B-SFX: FEET SPLASHING THROUGH LAKEWATER**

**(AT MASIKAS HOME)**

3. **C-SFX: SOUND OF BABY CRYING/ZAWADI.**

4. **BETTINA:** (**TRYING TO CALM BABY ZAWADI)**
Sssssh..zawadi..sssssh nyamaza toto wacha kulia... una nini totoo?.... kila mtu anakuwa mgonjwa kwani kuna nuksi gani katika nyumba yangu? Ni nani anayenitegea haya? Nimechoshwa na maradhi haya!

5. **D-SFX: DOOR OPENS, FOOTSEPS**

6. **BETTINA:** Wajisikiaje mwanangu karembo? Wataka chochote nikupatie?

7. **KAREMBO:** **(WEAK SICKLY VOICE)**
Ia mama... nataka kwenda msalani... jana sikupata hata lepe la usingizi... nilisikia baridi kisha zawadi pia alilia sana... kwani pia yeye anaumwa?

8. **BETTINA:** Sifahamu.. alianza kulia mapema jana.. na usiku .. tulikaa macho kucha... hataki hata kunyonya! Maziwa yangu ameyasusia kabisa! Na kipaji chake kiko moto ajabu!

9. **KAREMBO:** Najihisi mchovu na mnyonge! Pia nahisi kisunzi...

10. **BETTINA:** Kisunzi ni kwa sababu huli chochote... na ulacho unakitapika... lakini mamake david amesema utapata afueni...

11. **KAREMBO:** Mamake David? Tangu lini akawa daktari? Na atajuwaje nitapata nafuu bila ya kunifanyia utafiti au hata kuniona hali yangu?

12. **BETTINA:** **:** Anajuwa... yeye ni mtaalamu.. ana uzoefu na mambo mengi... hata huoni homa yako imeanza kupunguwa? Au sivyo?

13. **E-SFX: BABY CRYS AGAIN.**

14. **BETTINA:** Ssh! Sssh! Usilie mwanangu mzuri... Karembo hebu nenda ukaoge.. nataka nikusuuzie japo uji upate kunywa...

15. **F-SFX: DOOR OPENS, CLOSES**

**NARRATOR:** Tunapoangazia maradhi yeyote... kumbuka kuwa dalili au ishara zinapozidi ni muhimu kumuona daktari ili upate ushauri mzuri wa kimatibabu. Unapofanya hivyo utahakikisha kuwa unajihifadhia chembechembe zako za damu ya kupambana na maradhi na kujiepusha na ugonjwa wa anemia au ukausha damu... na iwapo matibabu kabambe hayatapatikana basi unahatarisha kuuguwa figo,malaria kali... au hata kifo. Karembo kweli anafahamu haya yote? Na je Zawadi ni kweli ameambukizwa

malaria? Yote hayo tutapata jawabu lake lakini kwanza tumuangazie Masika alipofikisha shehena yake ya samaki kwa mamake david.

**SCENE TWO: MASIKA AT MAMA DAVID'S HOUSE**

16. **G-SFX: DOOR BEING KNOCKED.**

17. **MASIKA:** Habari mamake david... samaki kutoka ziwani , kuingia kwenye nyavu na punde wataelekea chunguni mwako! Sema fungu ngapi? **(CHUCKLES LIGHTLY)**

18. **MAMA DAVID:** Ah! Karibu masika umeniletea vumba leo au samaki?

19. **MASIKA:** **(SHY)**
sidhani kama hiyo ni busara , tusiwape waja faida wakatusimanga bure.....

20. **MAMA DAVID:** **(NOW SHE LAUGHS)**
Sawa, upendavyo.haya umeniletea nini?

21. **H-SFX: BASKET BEING OPENED**

22. **MAMA DAVID:** **(SHOCKED)**
Sasa umekwenda kuniokotea uduvi huu? Hawa si ni watoto wa samaki.. wazazi wao wako wapi?**(LAUGHS MORE)**

23. **MASIKA:** **(GETTING IMPATIENT AND AGITATED)** sasa utanunuwa au utawatazama kama picha? Sikuja hapa kupiga gumzo.. tena unajuwa nina binti mgonjwa nyumbani.. nina haraka ya kwenda kumuangalia nijuwe hali yake inaendeleaje...

24. **MAMA DAVID:** Basi hutaniwi? Mbona hasira nyingi asubuhi hii?hebu changamka siku bado changa.

25. **MASIKA:** Hapana! Nitafanyaje wakati nina binti mgonjwa na kale kachanga nacho kanalia usiku mzima... na sina wasaa mzuri wa kuuza samaki wangu kwa sababu ya kuwahudumia...

26. **MAMA DAVID:** Kwani Karembo bado anaumwa? Hakuenda shule?

27. **MASIKA:** Ana takriban wiki moja sasa hajakwenda... nimempa kila aina ya tembe za malaria lakini bado afya yake inadhoofika kila uchao...

28. **MAMA DAVID:** Hebu tuandamane... nilimuahidi betina nitampitia... haya niuzie hivyo vizeri kidogo kisha tuandamane.. sawa? Au bado waogopa majirani watasema?

29. **MASIKA:** Hapana,nitakusubiri hapa nje... nikufungie wangapi?

30. **I-SFX: BASKET/PLASTIC BAG BEING OPENED**

31. **MAMA DAVID:** **(SELECTING)**
huyu, huyu hapa.. na huyu.. hapana hicho usiniwekee... huyo mwenye sura mbaya simtaki... enheee... huyo sawa... sasa hao tosha...

32. **J-SFX: SOMETHING BEING WRAPPED IN PAPER.**

33. **MASIKA:** Hao watakuwa ni shilingi ishirini..... lakini fadhila za kutukopesha mafuta ya taa siku ile nitakupunguzia shilingi tano... nipe shilingi kumi na tano...

34. **MAMA DAVID:** Nashukuru, subiri nikuletee pesa halafu twende..

**NARRATOR:** Huku masika na mamake david wakielekea nyumbani kwa masika kumuangalia karembo .. kule shuleni anakosoma karembo tayari mwalimu mkuu alikuwa ameingiwa na wasiwasi kwa kutomuona Karembo zaidi ya wiki moja shuleni.

**<u>SCENE THREE: AT KAREMBO'S SCHOOL,H/TEACHER IN CLASS</u>**

35. **K-SFX: NOISY VOICES FROM YOUNG STUDENTS**

36. **H/TEACHER:** Kimya! Ni nani anafahamu karembo anaendeleaje na ugonjwa wake hivi sasa? Limepita juma sasa na sijapata arafa yeyote kumuhusu... david.. wewe ni jirani yake... una

habari yeyote?

37. **DAVID:** La.. sijamuona kwa muda sasa.. mwalimu..

38. **H/TEACHER:** Inakuwaje na nyinyi hutembea pamoja kutoka shule?

39. **L-SFX: CHEERS AND CLAPS FROM CLASS**

40. **H/TEACHER:** Kimya! Sikumaanisha chochote kibaya... nilitaka kujuwa maendeleo ya karembo baada ya kuondoka hapa akiwa mgonjwa... na nyinyi munajuwa tumewahi hapo siku za nyuma kupoteza watoto wengi hapa shuleni kwa malaria.. na wenzenu wengi ni mayatima kwa ajili ya malaria..itakuwa pigo kubwa iwapo chochote kitamtokea karembo wakati huu ambapo tunajiandaa kwa mtihani wa mwisho...

41. **DAVID:** Mwalimu, basi nitapitia na kwao leo baada ya shule alafu kesho nitakupa taarifa yake..

42. **H/TEACHER:** vyema! Kwa sasa ningewauliza nyote muwe na tahadhari katika msimu huu wa mvua ili kujiepusha na malaria...

43. **DAVID:** Mimi huchoma na kufukiza dawa ya mbu kila mara nyumbani lakini mamangu halipendelei hili... kuna njia nyengine swadakta ya kutumia kufukuza

mbu?

44. **H/TEACHER:** Mimi si mtaalamu lakini naahidi kuwaletea mtaalamu hapa shule hivi karibuni.. awazungumzie.. lakini ninajuwa ni muhimu aidha kupuliza dawa ya kuua wadudu au kulala chini ya neti iliyotibiwa na dawa ya kuua na kufukuza mbu.. ukosapo hayo, basi vaa mavazi ya mikono mirefu na surwale ndefu hasa nyakati za jioni na usiku saa ambazo mbu huja kufyonza damu yenu.utumiaji wa DDT haupendekezwi kwani unaweza kudhuru afya.

45. **K-SFX: SCHOOL BELL RINGS/NOISE FROM STUDENTS**

46. **H/TEACHER:** Jambo jengine muhimu kwa sisi tunaoketikaribu na mito, mabwawa au sehemu zinazoketi maji.. nilazima tukate kichaka kinachoweka makao ya mbu hao... au kuondosha maji hayo ili mbu wasitage mayai hapo na kuwavamia..

**NARRATOR:** Maelezo ya mwalimu mkuu kuhusu kinga ya malaria yalimwingia David vizuri na akamfikiria tena karembo.. kengele ilipopigwa tu, alichomoka mbio kuelekea kwa kina karembo.. huku nako mamake david akiwa na betina walikuwa wakipeana mawazo jinsi watakavyo fanya kwani hali ya karembo ilizidi kuwa mbaya.

**<u>SCENE FOUR:AROUND THE TABLE AT MASIKAS HOME</u>**

47. **L-SFX: VEGETABLES BEING CHOPPED ON A BOARD**

48. **MAMA DAVID:** Hebu nikuchambulie hivyo vitunguu.. mwanamke hana ugeni.. mwili wangu pia ushazoea kazi..

49. **BETTINA:** Labda ukamwangalie zawadi amelala dakika chache kabla uje na mumewangu...ndiokuchelewa huku... sikulifumba jicho langu usiku kucha... na mchana sikuwahi pia..

50. **MAMA DAVID:** Wewe humkingi mtoto na jinamizi au maruhani... hee basi kila siku atakusumbuwa na yeye pia atasumbuka.. hebu mpeleke kwa mizanja.. yule mganga.. atampa mvuje na mafunsho mengine ya kumkinga na hutababaika tena...

51. **BETTINA:** **(UNSURE)**
sina hakika, mumewangu haamini itikadi hizo..sasa huyu mtoto bado mchanga zawadi atadhuriwa na jinamizi gani jamani?

52. **MAMA DAVID:** Ewe! Wasemanini? Betina mbona wataka kunishangaza? sisi niwaafrika... mapepo yapo! Na macho ya dege pia yapo! Ukitaka kuwaua wanao sawa! Lakini nishakwambia... wapeleke zawadi na karembo kwa mganga!!!

53. **. BETTINA:** **(SHOCKED)**

Ati?, Karembo pia? Mwanangu yule na elimu yake na hivi alivyokuwa.. hatakubali! Namjua binti yangu yule alivyo mkaidi...

54. **MAMA DAVID:** Mwenzangu nakuibia siri... mumeo na wangu walikuwa wote wavuvi na sikudanganyi nimetazamia nikaona karembo wako watu hawamuangalii kwa uzuri kwa hivyo ni mpaka ujifunge kibwebwe mwenzangu la sivyo utamkosa...

55. **BETTINA:** **(THINKING, TAKES DEEP BREATH)** Eh ni kweli! lakini tusimueleze mume wangu... nitamfanyia ...

56. **MAMA DAVID:** Hilo tushalifundika... mja ni siri bwanawe... kwanza yuko wapi huyo mumeo?

57. **BETTINA:** Nafikiri yuko chumbani anasikiza redio ..

58. **M-SFX: BABY STARTS TO CRY AGAIN**

59. **BETTINA:** Basi utiriri huu ameuanza tangu jana..hatupumui

60. **N-SFX: KNOCKING ON DOOR**

61. **MAMA DAVID:** Kwani watarajia wageni?

62. **BETTINA:** Hasha! Labda anijie ghafula ..

63. **DAVID:** Ni mimi david... nimekuja kumtazama karembo... hodi!!!

64. **MAMA DAVID:** Mmmh (**WHISPERS)**
Ala! Mwanangu David? Na Karembo? Mbona kwangu haya ni mageni?

65. **BETTINA:** Pia mimi siyajui hayo... nijuavyo wanasoma pamoja na kuishi karibu.. basi!

66. **MAMA DAVID:** Sawa... siongezi kitu hapo... basi si umkaribishe...

67. **BETTINA:** Ingia... hujambo david? Habari ya shule?

68. **DAVID:** Nzuri... lakini nimempeza karembo...nimekuja kumtembelea
(**REALISES IT MIGHT HAVE SOUNDED AMBIGUOUS)**
kuhusu mambo ya shule.. tulisoma kitu nataka nimueleze... yuko wapi? Anaendeleaje na homa?

69. **BETTINA:** Hajisikii vizuri... ngoja niwaone yeye na zawadi kwanza..

70. **MAMA DAVID:** Kwahivyo kila ukitoka shule mpaka upitie huku kwanza?

71. **DAVID:** Tafadhali mama,tusianze ugomvi..

72. **O-SFX: SOUNDS OF MOSQUITOES BUZZING AROUND**

**NARRATOR:Mpaka hapo ndio tumefika mwisho wa** kipindi chetu cha nne katika mzozano wa mamake david na mwanawe. Je, david atamueleza karembo kuhusu maambukizi ya mbu? Na karembo atakuwa na maamuzi gani? Je, betina atamzidi ujanja mumewe na kuwapeleka watoto kwa mganga? Kwa haya na mengineyo jiunge nasi katika kipindi kijacho cha **"WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA DHIDI YA MALARIA**"

unapotaka kusikiza tena au kutuma maoni yako tembelea tovuti zetu www.dw-world.de/lbe